**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI**

**Kumb.Na.BA.1/25/01A/14** **20 Febuari, 2026**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Tume ya Utumishi Serikalini inatangaza nafasi za kazi kwa ajili ya Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar kama ifuatavyo:

**1. Afisa Mthamini Daraja la II (ZPSH-10)** ***Nafasi 4 – Unguja***

***Sifa za Muombaji:***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Uthamini Mali (Land Management and Valuation) kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**2. Afisa Usimamizi wa Mali Daraja la II (ZPSH-10)** ***Nafasi 2 - Unguja***

***Sifa za Muombaji:***

- Awe ni Mzanzibar mwenye umri usiozidi miaka 46.
- Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Usimamizi wa Mali au Uongozi wa Fedha au Fedha na Uwekezaji (Real Estate Financial and Investment) kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**3. Afisa TEHAMA (Computer Programmer) Daraja la II - (ZPSH-10)** ***Nafasi 3 Unguja***

***Sifa za Waombaji:***

- Awe Mzanzibari, mwenye umri usiozidi miaka 46
- Awe aliehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Sayansi ya Kompyuta, Uhandisi wa Kompyuta, Uhandisi wa Programu, Teknolojia ya Habari kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**4. Afisa TEHAMA (System Analyst) Daraja la II (ZPSH-10)** ***Nafasi 1 Unguja***

***Sifa za Waombaji:***

- Awe Mzanzibari, Mwenye umri usiozidi miaka 46
- Awe amehitimu shahada ya kwanza katika fani ya Sayansi ya Kompyuta, Uhandisi wa Kompyuta, Uhandisi wa Programu, Usalama wa Mifumo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

***Jinsi ya Kuomba:***

- Maombi yote yawasilishwe kwa njia ya Kielektroniki kwenye mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira) kupitia anuani ifuatayo: **https://portal.zanajira.go.tz** kuanzia tarehe **20 Febuari, 2026 hadi tarehe 01 Machi, 2026.**
- Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Tume ya Utumishi Serikalini **www.zanajira.go.tz**.

- Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo kupitia mfumo wa ZanAjira (kwa njia ya kielektroniki pekee):-

  **KATIBU,**

  **TUME YA UTUMISHI SERIKALINI,**

  **S.L.P 1587,**

  **ZANZIBAR**
- Muombaji anatakiwa kuainisha nafasi ya kazi anayoiomba.
- Muombaji atakaewasilisha "Progressive Report" au "Statement of Results" pekee maombi yake hayatazingatiwa.
- Kwa msaada wa kitaalamu wasiliana na Tume ya Utumishi Serikalini kupitia simu Nam. 0773101012.

**LIMETOLEWA NA:**
**KATIBU,**
**TUME YA UTUMISHI SERIKALINI.**